Nimefanya Nini?

(What Have I Done?)

Na

Ellis P. Forsman

Nimefanya Nini?

(What Have I Done?)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 17, 2011

Nimefanya Nini?

Yer. 8:1-13

Yer. 8:1-13, "*Wakati ule asema BWANA watatoa mifupa ya wafalme wa Yuda, na mifupa ya wakuu wake, na mifupa ya makuhani, na mifupa ya manabii, na mifupa ya wenyeji wa Yerusalemu, itoke makaburini mwao; nao wataitawanya mbele ya jua, na mwezi, na jeshi lote la mbinguni walivyovipenda, na kuvitumikia na kuandamana navyo, na kuvitafuta, na kuviabudu haitakusanywa pamoja tena, wala kuzikwa; itakuwa ni samadi juu ya uso wan chi. Na kufa kutachaguliwa kuliko kuishi na mabaki yote waliosalia katika jamaa hii mbovu, waliosalia kila mahali nilikowafukuza, asema BWANA wa majeshi. Tena utawaambia BWANA asema hivi, je watu wataanguka wasisimame tena? Je mtu atageuka aende zake, asirudi tena? Mbona basi watu hawa wa Yerusalemu wamegeuka waende nyuma, wasikome kugeuka hivyo? Hushika udanganyifu sana, hukataa kurudi. Nalisikiliza nikasikia, lakini walisema yasiyo sawa; hapana mtu aliye tubia maovu yake, akisema* ***nimefanya nini?*** *Kila mtu hurudia mwendo wake mwenyewe, kama farasi aendavyo kasi vitani. Naam, koikoi angani ajua nyakati zake zilizoamriwa; na huwa na mbayuwayu na korongo huangalia wakati wa kuja kwao, bali watu wangu hawazijuia amri za BWANA. Mwasemaje sisi tuna akili na torati ya BWANA tunayo pamoja nasi? Lakini tazama kalamu yenye uongo ya waandishi imefanya kuwa uongo. Wenye hekima wametahayari, wamefadhaika na kushikwa; tazama wamelikataa neno la BWANA, wana akili gani ndani yao? Basi kwa hiyo nitawapa watu wengine wake zao na mashaamba yao nitawapa wale watakao wamiliki; maana kila mmoja wao, tangu aliye mdogo hata aliye mkubwa, ni mtamanifu; tangu nabii hata kuhani, kila mmoja hutenda mambo ya udanganyifu. Kwa maana wameiponya jeraha ya binti ya watu wangu kwa juu juu tu, wakisema, Amani, Amani, wala hapana amani. Je walitahayarika, walipokuwa wametenda machukizo? La! Hawakutahayarika wala hawakuweza kuona haya usoni; basi wataanguka miongoni mwao waangukao; wakati wa kujiliwa kwao wataangushwa chini, asema BWANA. nitawaangamiza kabisa, asema BWANA; hapana zabibu katika mizabibu, wala tini katika mitini, hata jani lake litanyauka; na vitu vile nilivyowapa vitawapotea.*"

Mwanafunzi aliitwa kwenye ofisi ya mkurugenzi. Alipofika aliuza, "Nimefanya nini?"

Hili ni swali linalorudiwa kila mara.

Polisi wanaulizwa swali hili mara nyingi kila juma.

Katika Agano la Kale watu wa Mungu hawakujali kile walichofanya kibaya.

Yer. 8:6, "*Nalisikiliza nikasikia, lakini walisemaa yasiyo sawa; hapana mtu aliyetubia maovu yake**, akisema nimefanya nini?*** *Kila mtu hurudia mwendo wake mwenyewe, kama farasi aendavyo kasi vitani.*"

Walikuwa katika marefu ya dhambi.

Yer. 8:5, "*Mbona basi watu hawa wa Yerusalemu wamegeuka waende nyuma, wasikome kugeuka hivyo? Husshika udaanganyifu sana, hukataa kurudi.*"

Nataka kuuliza baadhi ya maswali kuhusu sehemu tofauti, na ujiulize mwenyewe, "Nimefanya Nini?"

Umefanya nini kiroho?

Umetenda dhambi.

- 1 Yoh. 1:8-10, "*Tukisema kwamba hatuna dhaambi twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo ndani mwetu. Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata aatuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. Tukisema kwamba hatukutenda dhambi, twamfanya yeye kuwa mwongo wala neno lake halimo mwetu.*"
- Rum. 3:10, "*Kama ilivyoandikwa ya kwamba, hakuna mwenye haki hata mmoja.*"
- Rum. 3:23, "*Kwa sababu wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.*"
- 1 Yoh. 3:4, "*Kila atendaye dhambi afaanya uasi; kwa kuwa dhambi ni uasi.*"

Umejitenga mwenyewe na Mungu.

- Efe. 2:1-3, "*Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu; ambazzo mlizitenda zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa kaatika wana wa kuasi; ambao zamani sisi ssote nasi tulienenda kati yao katika tamaa za miili yetu, tulipoyatimiza mapenzi ya mwili na ya nia, tukawa kwa tabia yetu watoto wa hasira kama na hao wengine.*"

- Isa. 59: 1-2, "*Tazama mkono wa BWANA haukupunguka, hata usiweze kuwaokoa wala sikio lake si zito, hata lisiweze kusikia; lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone, hata hataki kusikia.*"

Umetii injili au umeikataa.

Ni uwezo wa Mungu.

Rum. 1:16, "*Kwa maana ssiionei haya injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia.*"

Inapaswa kuheshimiwa.

- Heb. 5:8-9, "*Na ingawa ni Mwana, alijifunza kutii kwa mates ohayo yaliyompata; naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii;*"
- Yoh. 14:15, "*Mkinipenda mtazishika amri zangu.*"

Hakuna sehemu rahisi.

Umefanya nini na Yesu Kristo?

Je unampenda?

Je yeye ni kiongozi wako, rafiki, mpatanishi?

Je yeye ni Mwokozi wako?

Mat. 1:21, "*Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.*"

Je umemtii?

Heb.5:9, "*Naye alipokwisha kukamilishwa akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii.*"

Umelifanyia nini Biblia?

Ambacho wengine wamefanya:

Wamelikataa.

Wameliacha kaabatini.

Binti mdogo wakati fulani aliulizwa, "je unaifahamu Biblia yako?" "Oh, ndiyo mkuu!" "Unaweza kuniambia kilichomo ndani yake?" "Naweza kukwambia kila kitu kilichomo ndani yake." "Oh, wangu! Niambie sasa." "Picha ya rafiki wa kiume wa dada yangu imo ndani yake; na risiti ya familia ya mama yangu pia imo ndani

yake; na kifungashio cha nywele zangu nilipokuwa mdogo pia kimo ndani yake.

Kuifanya rahisi.

- Ndege anaweza kukaa kwa siku 9 bila chakula.
- Mwanadamu siku 12.
- Mbwa siku 20.
- Kasa siku 500.

Lakini chaakula ni mhimu kwa viumbe vyote.

Kuna baadhi ya "ndege" Wakristo wanaokaa zaidi ya siku 9 bila kuwa na chakula cha kiroho.

Na kuna "kasa" wengine Wakristo wanaokaa zaidi ya siku 500 bila kuwa na chakula cha kiroho.

Sisi ni Wakristo wa aina gani?

Hatuielewi.

Tunachopaswa kulifanyia.

Kujifunza.

2 Tim. 2:15, "*Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.*"

Tuiheshimu.

Mat. 4:4, "*Naye akajibu akasema, imeandikwa mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.*"

Tuiweke katika mioyo yetu.

Zaburi 119:97-104, "*Sheria yako naipenda mno ajabu, ndiyo kutafakari kwangu mchaanaa kutwa. Maagizo yako hunitia hekima kuliko adui zangu, kwa maana ninayo siku zote. Ninazo akili kuliko wakufunzi wangu wote, maana shuhuda zako ndizo nizifikirizo. Ninao ufahamu kuliko wazee, kwa kuwa nimeyashika mausia yako. Nimeiepusha miguu yangu na kilaa njia mbaya, ili nilitii neno lako. Sikujiepusha na hukumu zako, maana wewe mwenyewe umenifundisha. Mausia yako ni matamu sana kwangu, kupita asali kinywani mwangu. Kwa mausia yako najipatia ufahamu, ndiyo maana naichukia kila njia ya uongo.*"

Tuiheshimu.

Yuda 1:3, "*Wapenzi nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu ambao ni wetu sisi sote, naliona imenilazimu kuwaandikia, ili niwaonye kwamba mwishindanie imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu.*"

Tuitii.

Heb. 5:9, "*Naye alipokwisha kukamilishwa akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii.*"

Umezifanyia nini karama zako?

Mat. 25:14-30, "*Maana ni mfano wa mtu atakaye kusafiri, aliwaita watumwa wake akaweka kwao mali zake. Akampa mmoja talanta tano, na mmoja talanta mbili, na mmoja talaanta moja; kila mtu kwa kadiri ya uwezo wake; akasafiri. Mara yule aliyepokea talaanta tano akaenda akafanya biashara nazo, akachuma faida talanta nyingine tano. Vile vile na yule mwenye mbili, yeye naye akachuma nyingine mbili faida. Lakini yule aliyepokea moja alikwenda akafukia chini, akaificha fedha ya bwana wake. Baada ya siku nyingi akaja bwana wa watumwa wale, akafanya hesabu nao. Akaja yule aliyepokea talanta tano, akaleta talanta nyingine tano, akisema Bwana, uliweka kwangu talanta tano; tazama talanta nyingine tano nilizopata faida. Bwana wake akamwambia, vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako. Akaja na yule aliyepokea talanta mbili, aksema Bwana uliweka kwangu talanta mbili; tazama, talanta nyingine mbili nilizopata faida. Bwana wake akamwambia vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako. Akaja na yule aliyepokea talanta moja, akasema Bwana nalitambua ya kuwa wewe u mtu mgumu, wavuna usipopanda, wakusanya usipotawanya; basi nikaogopa nikaenda nikaificha talantaa yako katika ardhi; tazama unayo iliyo yako. Bwana wake akajibu akamwambia, wewe mtumwa mbaya na mlegevu, ulijua ya kuwa navuna nisipopanda, nakusanya nisipotawanya; basi, ilikupasa kuiweka fedha yangu kwa watoa riba; nami nikija ningalipata iliyo yangu na faida yake. Basi mnyang'anyeni talanta hiyo, mpeni yule aliye nazo talanta kumi. Kwa maana kila mwenye kitu atapewa, na kuongezewa tele; lakini asiye na kitu, hata kile alicho nacho atanyang'anywa. Na mtumwa yule asiyefaa mtupeni mbali katika giza la nje; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno.*"

Umezifanyia nini nafasi zako?

Tunakabiliana nazo kila siku.

Kuwafundisha wengine kuhusu Yesu.

Marko 16:15, "*Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.*"

Tuwafundishe ndugu zetu, tuliyosoma nao, marafiki, wafanya kazi wenzetu, majirani n.k.

Sote tuna nafasi. Kwa wengine, nafasi hizi labda haziwezi kuja tena.

Hitimisho

Umefanya nini?

Hili ni swali kuu.

Kuna lililo kubwa zaidi.

Utafanya nini kwanzia sasa na kuendelea?

Je wewe ni Mkristo? Zifuatazo ni hatua mhimu ya kufanyika mmoja:

- **Imani.** Waeb. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa dhawabu wale wamtafutao." Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na mimi akniambia kwamba haamini kwamba Mungu yuko. Kwa vile nilisha batizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu mandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya ukristo ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamba Mungu yuko. Lakini ili kuwa upande salama, labda anapaswa kwenda kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani atampeleka mbinguni (kama kuna mbingu), na si motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.*"
- **Toba.** Matend. 2:38, "*Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" Matend 11:18, "*...Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima.*" Kama ulikuwa unalala,

ukasikia kelele kwenye chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "Kwamba kuna mwizi!" taratibu unachukua simu ya mkononi, unawapigia polisi. Kidogo polisi wanafika na kumshika mwizi. Alafu anapiga kelele, "samahani; samahani!" Anaomba msamaha wa nini? Kwa sababu amekamatwa; si kwamba ameiba. Toba iliyokweli ni kwamba mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena. Hiyo ndio toba ya kweli. Ni badiliko la nia linaloleta badiliko la matendo. Tunatakiwa kufanya hivyo kabla hatujawa wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*"

  Tuna kiri nini? Kwamba tuna amini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu.

  Kumbuka kwamba katika andiko hilo hapo juu kwamba imani (kuamini), toba, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" inamanisha kuelekeza kwenye kitu Fulani; si kwamba mtu ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu mwenyewe alibatizwa kuitimiza haki yote, "*Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, huyu ni mwanangu mpendwa, ninaye pendezwa naye.*" (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo sahihi la kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema, "*Imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote.*" Tuna batizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, si kwa sababu ni haki yetu.

  Kwa kweli, tusipo batizwa, tungali katika dhambi zetu. "*Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" (Matend. 2:38). Petro, umesema kusudi la ubatizo ni nini? "*Kwa ajili ya ondoleo la dhambi*".

Kwa nini watu wanapenda kuach hatua inayotuondoa dhambi zetu?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tubatizwe. "*Na akawambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye* ***na*** *kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*" (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu iki hiki, "*Unakawilia nini? Simama, na ubatizwe, na uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Matend. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko, "Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima." (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale umekufa. "Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake. Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlvyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika katika mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusiitumikie dhambi tena." (Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumiwa na damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru na dhambi zetu za zamani kama tu tukibatizwa.

Hii haimanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuwezi kupeleka maiti makaburini, na kumwekea udongo kidogo juu yake; tunauzika mwili.

Kama hujafanyika Mkristo, kwa nini usifanyike leo?